
SWAHILI

3162/01

Paper 1

May/June 2019

3 hours

No Additional Materials are required.

READ THESE INSTRUCTIONS FIRST

An answer booklet is provided inside this question paper. You should follow the instructions on the front cover of the answer booklet. If you need additional answer paper, ask the invigilator for a continuation booklet.

Answer **all** questions.

The number of marks is given in brackets [] at the end of each question or part question.



This document consists of **6** printed pages, **2** blank pages and **1** Insert.

1 Translate the following passage into **English**:

Kwa kawaida, Zuberi huamka asubuhi na mapema, hukoga, huvaa sare zake za shule halafu hunywa chai. Baadaye Zuberi huchukua mkoba wake wa shule na hukimbia kwenda kwenye kituo cha mabasi.

Kituo hicho ni kipya, kikubwa na cha kisasa. Kimejengwa kwa ajili ya mabasi ya mwendo kasi. Mabasi haya husafiri kwenye barabara maalumu ambazo hazina foleni. Magari mengine hayaruhusiwi kutumia barabara hizo. Kwa hivyo Zuberi hufika shuleni mapema sana.

Zamani, Zuberi alisafiri kwa mabasi ya kienyeji na ilimchukua dakika hamsini kutoka nyumbani hadi shuleni. Siku hizi safari hiyo hiyo inachukua dakika ishirini tu. Anapofika shuleni Zuberi anakuwa na muda wa kuzungumza na wanafunzi wengine na kujitayarisha kwa masomo yake ya siku hiyo.

Pia anapokuwa ndani ya basi la mwendo kasi, Zuberi anapata kiti cha kukalia. Yeye anapendelea kiti kilicho karibu na dirisha ili aweze kuangalia zogo la asubuhi huku akiwa amestarehe.

[20]

2 Translate the following passage into **Swahili**:

Today, I washed, ironed and folded my best clothes, before packing them in the old black suitcase that my mother has lent me for the trip.

Tomorrow morning, I will be leaving Nairobi for the first time and flying to Mombasa to see my cousins. My parents wanted me to travel by plane, as they said it would be faster and less tiring. I am disappointed I won't be going by train, as my friend Hannah did a few weeks ago.

Hannah told me that the train is a great way to see some really beautiful scenery. She also saw a lot of animals as the train passed through the Tsavo National Park. She didn't see any lions, but she did manage to spot zebras, giraffes and gazelles. Hannah said that the train also crossed through villages, and that children would often cheer and chase the train while waving at the passengers. She called it one of the most beautiful trips she has ever taken. I would have been really happy to have seen everything she described to me.

However, I am still very excited to see Mombasa, to be with my family and to wear all my best outfits! My plan is to visit the historical Fort Jesus, walk around the old town and also to relax on the beach. Even without travelling by train, I know I will still enjoy my holiday.

[30]

3 Read the text and answer the questions that follow in **Swahili**.

Kuna mashindano mengi yanayoendeshwa shuleni kwetu ingawa kwa kawaida haya huwa ni ya michezo, muziki na midahalo. Mimi sijawahi kuingia kwenye shindano lolote kwani huhisi haya kuwa mbele ya umati wa watu. Lakini, mwezi uliopita Mwalimu Mkuu alitangaza shindano la uandishi wa ushairi. Nilifurahi sana kwani kwa muda mrefu nimekuwa nikiandika mashairi na kuwapa ndugu zangu wasome. Wote wamekuwa wakinisifia sana, kwa hivyo ninajua kwamba uwezo ninao. Tena mara kwa mara baba yangu husema “Juma, ipo siku utakuwa mshairi maarufu sana duniani kote”. Maneno hayo yamekuwa yakinipa motisha sana. Sasa muda umewadia kwa mimi kuonyesha kipaji changu. Nilichapa kazi usiku na mchana ili kutunga shairi zuri sana.

Lakini jana nilipofika shuleni niliona tangazo ukutani lililonivunja moyo sana. Mashindano yalikuwa yamefutwa kwa sababu watu wawili tu kati ya wanafunzi mia tano shuleni kwetu ndiyo waliokuwa wametuma mashairi yao. Nilijihisi kama ndege aliyevunjwa mbawa. Nilijisikia uchungu kwamba wanafunzi wenzangu wote wanataka kupoteza muda wao wakisikiliza Bongo Flewa na kuzitia picha zao kwenye mitandao ya kijamii au wakirusha mipira uwanjani.

Baada ya shule, nilipokuwa narudi nyumbani, nikamwona rafiki yangu Roza akipiga danadana na mpira wa mguu kwenye uwanja wa michezo. Nilisimama kumwalia pale uwanjani akionyesha ujuzi wake. Aliuambia mpira kama duma porini anapomnyemelea swala. Laiti na mimi ningaliweza kuonyesha ujuzi wangu kwenye ushairi kama yeye kwenye mpira.

Baada ya muda, aliniona na akaja kuniuliza kama ningependa kucheza mpira. “Hapana, sina hamu kabisa. Pia, mimi si mchezaji wa mpira bali mshairi” nilimjibu. “Kumbe wewe una mambo ya kishamba kweli!” akasema akicheka. “Ushamba kutunga mashairi au kukimbiza mpira uwanjani?” nikamwuliza “kwani kukimbiza mpira huu kunahitaji uwezo wowote? Hauna maana yoyote!” “Ala! Kumbe ndiyo maana ulikuwa unaniambia” Roza akajibu huku anacheka. Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu sikuwa na jibu la kutoa. Aliyosema yalinichoma moyoni. Nikakaa kimya na kufikiria kimoyo moyo “utaona!” Baada ya muda nilimwaga na kuondoka.

Sikuzungumza na Roza kwa muda mrefu baada ya hapo na pia sikutunga shairi lolote kwani nilikuwa bado ninajihisi kama nimechanganyikiwa. Halafu siku moja nilisoma kuhusu mashindano ya ushairi kwenye gazeti la taifa. Mshindi angetunukiwa tuzo la ushairi na kupewa pesa nyingi. Pia shairi lake lingepigwa chapa kwenye gazeti na kitabu maalumu. Nilipoona tangazo hili, damu ilinichemka kwa furaha.

Shindano hilo lilikuwa na masharti mengi ambayo kwa kweli mimi niliyaona kuwa marahisi sana. Kwanza ilibidi kutunga shairi. Pili, tungo za mashairi hayo ziliruhusiwa kuwa za aina yoyote. Pia kulikuwa na uhuru wa kuchagua mada yoyote. Na mwisho, kila mshindani alitakiwa kupiga chapa kazi yake na si kuandika kwa mkono, yaani kwa kalamu. Niliposoma tangazo hilo nilijua kwamba kulikuwa na umuhimu kwangu kutunga shairi na kulituma. Hii ilikuwa nafasi mpya ya kuwafanya wazazi wangu wajivunie kuwa na kijana kama mimi.

Baada ya kutuma shairi langu, sikusikia chochote kwa muda mrefu. Nikahisi kwamba shairi langu halikufanikiwa. Nilishaanza kusahau kuhusu shindano hilo nilipofika shuleni asubuhi moja na kukuta watu wamejaa tele kwenye ukuta wa matangazo ya shule. Sikujua wanafanya nini hapo. Nilishangaa kuona watu wanakuja kunipongeza kwa kunigonga begani. Pole pole nikaanza kutembea kuelekea ukutani, moyo ukinidunda. Mbele ya tangazo nilimwona Roza akichekelea. Nilipofika ukutani nilikuta tangazo jipya juu ya lile la zamani ambalo lilihusu kufutwa kwa mashindano. Tangazo jipya lilikuwa ni kipande cha gazeti kilichokuwa na shairi. Shairi liliitwa “Duma Mchezaji”.

Mwalimu Mkuu alikuwa amesimama kando akitabasamu.

Now answer the following questions in your own words, as far as possible. You should avoid copying word-for-word from the text.

- (a) Kwa nini Juma alipata moyo kutuma shairi lake kwenye shindano lililotangazwa na mwalimu mkuu? Taja sababu **tatu** kutoka kwenye aya ya kwanza. [3]
- (b) Kuna ushahidi gani kwamba mashairi si maarufu shuleni? Taja maelezo **mawili**. [2]
- (c) Kwa nini Juma anajifananisha na ndege na anamlinganisha Roza na duma? Taja maelezo **mawili**. [2]
- (d) Kwa nini Juma anakaa kimya mwisho wa mazungumzo yake na Roza? Taja maelezo **mawili**. [2]
- (e) Kwa nini hisia za Juma zinabadilika baada ya kusoma gazeti? [1]
- (f) Juma atahitaji kufanya nini ili shairi lake likubalike kwenye shindano. Taja mahitaji **manne** kwa kutumia maneno yako. [4]
- (g) Kwa nini watu walimgonga Juma begani? [1]
- (h) Kwa nini Roza anachekelea? [1]
- (i) Kutokana na kifungu chote ulichokisoma, umefahamu nini kuhusu tabia za Juma na Roza. Toa maelezo **mawili** kwa Juma na pia toa maelezo **mawili** kwa Roza. [4]

[20 for Content + 5 for Language = 25]

- 4 Write a composition of about **120 words** in **Swahili** on **one** of the following topics:
- (a) The government has asked citizens to suggest improvements to your national museum, park and parliament. Choose **one** of these, and write about the changes you would like to see made.
 - (b) Imagine you are going to write a short television programme. What would it be about and why is the subject of the programme important to you?
 - (c) Write the first entry of a blog about the place where you live. [25]

BLANK PAGE

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge Assessment International Education is part of the Cambridge Assessment Group. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which itself is a department of the University of Cambridge.